



Utumwa wa Kisasa - Kenya

Hakuna Utambulisho, Hakuna Ulinzi: Hakuna anayejua niko hapa



**Freedom Fund
Modern Slavery
Credits**

Kenya

Produced with research from
African Migration and Development Policy Centre, United Nations University Centre for Policy
Research and the Freedom Fund

Researchers - Kenya

In Kenya, coordination was led by Dr. Linda Adhiambo Oucho, Veronica Mwangi, with support from Faith Wanjiku of AZADI Community, Peter Olewe of AZADI Community and David Muthama of the Refugee Legal Network.

Research Direction

Research support and oversight were provided by Professor Heaven Crawley and Angharad Smith.

Scriptwriter

Daniel Locke

Illustration

Daniel Locke

Translation

Veronica Mwangi

Production

PositiveNegatives

Director

Dr Benjamin Worku-Dix

Special Thanks to

We would also like to extend our thanks to the Freedom Fund, especially Débora Aranha, Jiyam Shrestha, Ruth Kimani, Varsha Gyawali, Dan Vexler, Havovi Wadia and Yuki Lo for their valuable guidance throughout this project.

Funded by

Freedom Fund

In Partnership with

United Nations University - Centre for Policy Research

Stories Drawn from Research

www.positivenegatives.org

@PosNegOrg



Hapa Kenya kuna watu wengi walio katika hatari ya utumwa wa kisasa ama ulanguzi wa binadamu. Janga hili linagusa Wakenya, Wahamiaji na jamii za wakimbizi...



Jamii za wahamiaji kutoka Afrika Mashariki huwa zina asili tofauti za kikabila na kitamaduni.




Ikiwemo Waeritrea, Waethiopia, Wasudani na Wasomalia.



Wakenya wengi na wahamiaji wamekumbana na matatizo katika kupata stakabadhi za uraia au vitambulisho vinavyotolewa na serikali.



Baadhi ya matatizo haya ni ya kihistoria...




... na uchelewaji unachangiwa na uhakiki wa muda mrefu na michakato ya uthibitishaji



Ukosefu wa stakabadhi au hati hizi una athari kubwa kwa maisha ya walioathirika.



Bila stakabadhi au hati hizi, watu hulazimishwa kuchukua kazi sisizo salama, na majukumu ya utumwa katika uchumi usio rasmi.




Ukosefu wa urasimu...

... Kutafsiri sheria vibaya ...



...matumizi ya sheria kubagua, kando na masuala haya, huwaweka watu wasio na stakabadhi hizi kwa hatari ya utumwa wa kisasa..



Nina umri wa miaka thelathini na nne (34), nimeishi*Kenya. Hii ndio nchi pekee ambayo nimewahi kujua, ninafanya kazi ya kufua nguo



Mimi ni kizazi cha nne (4) kwa familia yangu ambayo imekuwa bila stakabadhi/hati, ingawa tumeishi Kenya siku zote.



"Nilipozaliwa mamangu na babangu hawakuwa na stakabadhi/ hati zozote,, kwa hivyo nimeshindwa kutuma ombi la stakabadhi zangu."



Kufua nguo za watu, au kusafisha nyumba zao ndiyo kazi pekee ninayoweza kupata.



Watu hunitumia vibaya, lakini chaguolipi ninalo, ila kufanya kazi hii?



Sitendewi vyema na watu ninaowafanyia kazi.



Wananitesa kwa sababu sina njia ya kuthibitisha kuwa mimi ni Mkenya.



Zamani nimeshawahinyanyaswa kijinsia na watu niliokuwa nawafanyia kazi. Sikuwaambia walioko kwa mamlaka, sikuwa na imani kwamba wangenisaidia.



Ninafanya kazi kwa muda mrefu sana, wakati mwingine bila malipo yoyote.



Watu ninaowafanyia kazi, walikataa kunilipa ...




...Na ninapolalamika, wakaniambia kwamba wanaweza fanya kile wanachopenda...



kwa sababu walisema hakuna mtu aliyekuwa anajua kuwa niko pale.



Nilizaliwa nchini Kenya.



"Nilipokuwa mdogo
mama yangu alifariki na
nikabaki peke yangu.
Bado namkumbuka."



Kwa sababu hakuna mtu ambaye
angeweza kunitunza nilichukuliwa na
kituo cha watoto yatima, niliishi maisha
yangu ya utotoni huko.



Nilipoondoka kwenye kituo cha watoto
yatima taasisi hiyo haikunipa
stakabadhi/hati zangu rasmi
zilizothibitisha kuwa ninatoka Kenya ...




Kwa sababu hii siwezi
kupata stakabadhi/hati
zozote za kisheria.



Nina wasiwasi, watu
hunifikiria vibaya kwa sababu
niliishi katika kituo cha
watoto yatima.





Mimi asili yangu ni kutoka Ethiopia.



Nilikuja Kenya kutafuta usalama na hifadhi kama mkimbizi wakati kulikuwa na vita nyumbani.



Nyumbani nilikuwa na elimu ya kutosha. Nilipata digrii na nilikuwa nikitarajia maisha



Lakini hapa nafanya lolote niwezalo ili kupata pesa. Mara nyingi mimi hufanya kazi ya ujenzi.




Masharti ni magumu sana, wakati mwingine msimamizi ananipiga ili nifanye kazi zaidi, siwezi kumripoti kwa ofisa wa Serikali kwa sababu sina kitambulisho, kama mtu mzima sina ulinzi ulio na mtoto kwa mujibu wa kisheria.



Ninalipwa kidogo sana kwa juhudi zangu, mara nyingi nalipwa tu kwa chakula, na kulazimishwa kurudi kazini tena siku inayofuata.



Siwezi kupata kazi rasmi ingawa nina cheti cha uthibitisho wa kusajiliwa kama mkimbizi/mtafuta hifadhi, lakini sina kitambulisho cha wakimbizi.



Nahitaji stakabadhi/karatasi za kunisaidia kwa mambo haya, lakini mara nyingi waliokwamamlaka hutuchukulia tofauti; wanaamini mtu wa Sudan (mkimbizi) hana pesa.



Nimejaribu kuomba kitambulisho, lakini afisa wa serikali huwa anauliza hati tofauti, ilhali zingine hazitakiwi kisheria. Natamani niishi maisha yangu lakini nahitaji stakabadhi/karatasi rasmi ili nifanye kazi.



Katuni hii imetengenezwa na **Daniel Locke** na kutayarishwa na **PositiveNegatives** kutokana na utafiti uliofanywa na **African Migration and Development Policy Centre (AMADPOC)/Kituo cha Sera ya Uhamiaji na Maendeleo ya Afrika (AMADPOC)**, na **United Nations University Centre for Policy Research/Kituo cha Utafiti wa Sera cha Umoja wa Mataifa, kwa ushirikiano na Freedom Fund/Mfuko wa Uhuru.**

Utafiti uliofanywa nchini Kenya unaonyesha jinsi ukosefu wa kupata stakabadhi /hati rasmi kati ya raia na wahamiaji huweza kuongeza hatari yao ya utumwa wa kisasa. Utafiti huu unaonyesha kuwa ukosefu wa stakabadhi /nyaraka rasmi huzuia upatikanaji wa huduma muhimu na huongeza hatari za unyanyapa. Pia, unapendekeza sera zinazofaa ili kushungulikia changamoto hizi zinazojumuisha kijamii na kiuchumi.

Unaweza kujifunza zaidi kuhusu matokeo ya utafiti huu katika ripoti kamili yenye kichwa "Bila Kitambulisho Hakuna Ulinzi: Jinsi ukosefu wa stakabadhi rasmi/ nyaraka unasukuma watu kwa utumwa wa kisasa"

